JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

# SHERIA BULLETIN

Toleo la Kumi




## YALIYOMO


01 | Mama Samia apewa Tuzo na ACHPR

03 | Vyeti vya kuzaliwa Watoto Milioni Nane vyasajiliwa

05 | Ujenzi wa Jengo la Wizara Wafikia Asilimia 80


## BODI YA UHARIRI


**MARY MAKONDO**
Katibu Mkuu

**LUSAJO MWAKABUKU**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAJUMBE**
George Mwakyembe | William Mabusi | Rosemary Mlale

**WASANIFU WA KURASA:** Waziri Bosco | Richard Mwamakafu

# Mama Samia apewa Tuzo na ACHPR

**Na Lusajo Mwakabuku & Rosemary Mlale - Arusha**
– Arusha.



Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (kulia), Mhe. Janet Ratatouille Sallah-Njie akimkabidhi Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana tuzo kwa niaba ya Mhe. Rais Samia.

Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu imemtunukia Tuzo ya Heshima Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutambua mchango wake katika kutetea, kulinda na kuimarisha haki za binadamu katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Tuzo hiyo imepokelewa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana kwa niaba ya Mhe. Rais Samia wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Afrika na maadhimisho ya miaka 20 ya Itifaki ya Maputo kuhusu Haki za Wanawake yaliyofanyika Jijini Arusha tarehe 21 Oktoba, 2023.



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akielekea kupokea tuzo kwa niaba ya Mhe. Rais Samia wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Afrika na maadhimisho ya miaka 20 ya Itifaki ya Maputo.

Akieleza sababu za kumtunuku Mhe. Rais Dkt. Samia tuzo hiyo, Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Mhe. Janet Ratatouille Sallah-Njie amesema Mhe. Rais Dkt. Samia amekuwa kiongozi wa mfano Barani Afrika katika kusimamia na kuimarisha haki za binadamu kuanzia ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Amesema Mhe. Rais Samia amefanikiwa kusimamia haki za binadamu kwa kuimarisha usawa wa kijinsia nchini, kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya na elimu kwa wasichana, kuwawezesha wanawake kiuchumi, kupambana na ukatili wa kijinsia, kuimarisha demokrasia na maridhiano, uhuru wa kutoa maoni na uhuru wa Vyombo vya Habari.

Ameongeza kusema ni bahati ya pekee kwa Afrika kuadhimisha miaka 20 ya Itifaki ya Maputo ya Haki za Wanawake kwenye ardhi ambayo Rais wake ndiye mwanamke pekee mwenye wadhifa huo wa juu barani humo.

***"Hakuna namna bora ya kusherehekea miaka 20 ya Itifaki ya Maputo ya Haki za Wanawake zaidi ya kusherehekea hapa Tanzania ambapo Kiongozi wa nchi ndiye Rais pekee mwanamke barani Afrika. Tuna kila sababu ya kumtunuku tuzo hii siyo tu kwa sababu ni mwanamke bali pia ni kutokana na hatua kubwa za maendeleo alizopiga na mchango wake kwenye masuala ya haki za binadamu nchini kwake na kwenye medani za kimataifa," amesisitiza Mhe. Sallah-Njie***

Amesema nafasi ya Rais Samia ambaye anasimama kama balozi wa usawa wa kijinsia duniani ni chachu na mfano wa kuigwa kwa wanawake na wasichana wa Afrika katika kuwahamasisha na kuwatia moyo katika kufanyia kazi ndoto zao kwa kushinda vikwazo mbalimbali na kwamba wana uwezo wa kushika nafasi kubwa na za juu za uongozi.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo, Mhe. Balozi Dkt. Chana ameishukuru Tume hiyo kwa kumtunuku tuzo Mhe. Rais Dkt. Samia na kumwelezea Mhe. Rais kama mwanamke kiongozi shujaa, mtetezi wa haki za binadamu na watu, mchapakazi na mtoto wa Afrika ambaye ni mwelewa na ameleta maendeleo nchini.

Amesema katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia kumekuwa na kasi kubwa katika kuleta maendeleo na kuwezesha mifumo ya upatikanaji haki kwenye Nyanja mbalimbali ikiwemo utoaji wa haki huru, uhuru wa kujieleza, uhuru wa kuabudu, uhakika wa chakula, kuwawezesha vijana kujiajiri, uwezeshaji wanawake na kuanzishwa kwa mpango wa msaada wa kisheria wa Dkt. Samia.
Pia amesema katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita ya Mhe. Dkt. Samia idadi ya wanawake katika vyombo vya utoaji maamuzi ikiwemo Mahakama, Bunge na Serikalini kwa ujumla imeongezeka.

"Mhe. Dkt. Samia mara baada ya kuingia madarakani alianzisha falsafa ya R4 kwa maana ya maridhiano na upatanishi, ustahimilivu, mageuzi na ujenzi mpya. Utaratibu wenye lengo la kustawisha na kudumisha amani, umoja, undugu na maridhiano kwa wananchi ili kuchocea maendeleo," amesema Mhe. Balozi Chana.



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akitoa hotuba ya shukrani baada ya kupokea tuzo kwa niaba ya Mhe. Rais Samia wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Afrika na maadhimisho ya miaka 20 ya Itifaki ya Maputo.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo akihutubia kwenye Jukwaa la Kitaifa la Wadau wa juhudi dhidi ya rushwa, tarehe 04 Desemba, 2023 Jijini Dodoma.

# NCHI IKITAWALIWA NA RUSHWA HAIWEZI KUFIKIA MALENGO: BI. MAKONDO

**Na William Mabusi**
– WKS Dodoma

Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo amezitaka Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi kuweka mazingira ya kuzuia rushwa, kuepuka na kutokomeza vitendo vya rushwa nchini ili kuliwezesha taifa kufikia malengo mbalimbali iliyojiwekea katika kuleta maendeleo nchini.

Bi. Makondo ameyasema hayo alipokuwa akihutubia kwenye Jukwaa la Kitaifa la Wadau wa juhudi dhidi ya rushwa tarehe 04 Desemba, 2023 Jijini Dodoma lililo hudhuriwa na Wadau kutoka Serikalini, Sekta Binafsi na Viongozi wa Dini ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu nchini. Siku ya Maadili na Haki za Binadamu nchini Tanzania ni jumuisho ya siku mbili za Kimataifa ambazo ni siku ya Kupambana na Rushwa na Siku ya Haki za Binadamu.

"Sote tunaelewa rushwa ni adui mkubwa wa maendeleo, nchi ikitawaliwa na rushwa taifa haliwezi kufikia malengo ililojiwekea katika nyanja mbalimbali. Aidha, rushwa inakiuka haki za binadamu kwa kuwa ulaji rushwa unapokonya haki za binadamu na kusababisha huduma mbalimbali kutowafikia wananchi kwa wakati," alisema. Siku ya Maadili na Haki za Binadamu ambapo kwa mwaka huu uzinduzi wake umefanyika tarehe 3 Desemba, 2023 inaadhimishwa sanjari na shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanyika kwa Jukwaa la Kitaifa la wadau wa juhudi dhidi ya rushwa, Maadhimisho ya Wiki ya huduma kwa jamii yatakayofanyika kwenye viwanja vya Nyerere Square kuanzia tarehe 5 hadi siku ya kilele Desemba 10, 2023 ambapo wadau wa Serikali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayojihusisha na masuala ya maadili na haki za binadamu watatoa huduma mbalimbali, watajibu maswali kuhusu haki katika nyanja ya maadili, kuzuia na kupambana na rusha, utawala bora na haki za binadamu.

Ametaja shughuli nyingine kuwa ni utoaji wa elimu kupitia Vyombo mbalimbali vya Habari ili kuendelea kuuhabarisha umma juu ya umuhimu wa kuzingatia maadili, kutokujihusisha na rushwa na kuzingatia haki za binadamu.

Kwenye mjadala uliofanyika kwenye Jukwaa la Kitaifa la Wadau wa Juhudi dhidi ya rushwa washiriki wamesisitiza elimu kuhusu maadili mema kuendelea kutolewa ili jamii ijikite katika kufanya mambo mema vile vile wamewataka Watanzania kusimamia mali ya umma kama vile wanavyosimamia mali zao wenyewe kwa faida ya kizazi chetu kijacho na maendeleo ya nchi. Maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu kwa mwaka huu yamebeba kauli mbiu isemayo "Zingatia maadili, utu, uhuru na haki kwa watu wote kwa maendeleo endelevu."



Washiriki kwenye Jukwaa la Kitaifa la Wadau wa juhudi dhidi ya rushwa, wakisikiliza hotuba, tarehe 04 Desemba, 2023 Jijini Dodoma.




Meza Kuu kwenye picha ya pamoja na baadhi ya Watumishi wa Serikali kwenye Jukwaa la Kitaifa la Wadau wa juhudi dhidi ya rushwa, wakisikiliza hotuba, tarehe 04 Desemba, 2023 Jijini Dodoma.

# TANZANIA IMESAJILI NA KUTOA VYETI VYA KUZALIWA KWA WATOTO ZAIDI YA MILIONI NANE



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akizindua Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri chini ya miaka mitano, Desemba 08, 2023 katika viwanja vya Mbagala Zakhiem Jijini Dar es Salaam.




Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akihutubia wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri chini ya miaka mitano, Desemba 08, 2023 katika viwanja vya Mbagala Zakhiem Jijini Dar es Salaam.




Katibu Mkuu Wizira ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo akihutubia wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri chini ya miaka mitano, Desemba 08, 2023 katika viwanja vya Mbagala Zakhiem Jijini Dar es Salaam.

**Na Lusajo Mwakabuku &**
– Dar es Salaam.

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana amesema kuwa Watoto zaidi ya milioni 8.8 wamesajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa katika mikoa 26 ya Tanzania Bara kupitia Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri chini ya miaka mitano.

Mhe. Waziri Balozi Dkt. Pindi Chana ameyasema hayo wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mpango leo Desemba 08, 2023 katika viwanja vya Mbagala Zakhiem Jijini Dar es Salaam.



Wananchi wakipatiwa huduma ya Usajili wa Watoto wa Umri chini ya miaka mitano, Desemba 08, 2023 katika viwanja vya Mbagala Zakhiem Jijini Dar es Salaam.

Uzinduzi huu unahitimisha Mikoa 26 ya Tanzania bara ambapo Mkoa wa Dar es Salaam unatarajiwa kusajili jumla ya watoto 248,298 na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa bila ya malipo kupitia vituo 505 vya usajili ambavyo ni Vituo vya Afya na Ofisi za Watendaji wa Kata.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo amesema, mpango huo ulioanza jijini Mbeya mwaka 2013 na kuhitimishwa jijini Dar es Salaam ikiwa ni jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita ambayo imekuwa ikitenga bajeti ya utekelezaji wa majukumu hayo na kuhakikisha wananchi wanasogezewa huduma katika maeneo wanakoishi.

Ameongeza kuwa, mpango huo ni mfano wa maboresho kwa kuwa huduma zimesogezwa karibu na wananchi na kutumia teknolojia ya simu za mkononi ambayo inarahisisha upatikanaji wa takwimu za watoto wengi wanaosajiliwa ndani ya muda mfupi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri RITA Dkt. Amina Msengwa amesema kuwa mpango huo ulianzishwa na Serikali kupitia RITA kwa kundi hilo la kimkakati la watoto kwani mipango mingi ya maendeleo hutegemea takwimu sahihi na hivyo kupitia mpango huo utawezesha Serikali kupata takwimu sahihi kwa wakati.

Naye Kabidhi Wasii Mkuu Bw. Frank Kanyusi amesema, Lengo la Mpango huo ni kuongeza kasi ya ya Usajili na kutoa vyeti kwa watoto wa Umri chini ya miaka mitano pamoja na kusogeza huduma kwa wananchi kuanzia ngazi ya Kata.

"Chimbuko la mpango huu ni kasi ndogo ya usajili, Serikali kwa kushirikiana na wadau wakaleta mpango huu ili kuongeza kasi ya usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watanzania wote." Amesema.

Pia, amewashukuru wadau mbalimbali wa Kitaifa na Kimataifa ambao ni Serikali ya Canada, Shirika la kuhudumia watoto duniani UNICEF, Kampuni ya simu za mkononi Tigo na kuahidi kuendelea na ushirikiano katika utoaji wa huduma hiyo kwa wananchi.

# “UNYANYASAJI WA KIJINSIA HAUNA NAFASI KATIKA NCHI YETU” DKT. CHANA

**Na William Mabusi**
– WKS Dodoma.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akihutubia wakati akifungua Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, tarehe 06 Desemba, 2023 Jijini Dodoma.

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) amesema Tanzania inaweza kusonga mbele na kushinda vita dhidi ya Ukatili wa Kijinsia ikiwa wote tutazungumza na kupaza sauti kupinga Unyanyasaji wa kijinsia huku akiitaka jamii kushiriki kikamilifu katika kutoa ushahidi wa matukio ya unyanyasaji wa kijinsia mara inapotakiwa kufanya hivyo.

Ameziagiza Taasisi za dini na Wazee wa kimila, Wanahabari na Wadau wa Maendeleo na wananchi wote wawe tayari kuchukua hatua za maksudi kukomesha ukatili wa kijinsia kwenye jamii zetu kuanzia familia, makazini kwetu na kwenye jamii zetu kwa ujumla.

Dkt. Chana ameyasema hayo alipokuwa akifungua Maadhimidho ya siku 16 za Kupinga Ukatili dhidi ya Kijinsia, tarehe 06 Desemba, 2023 Jijini Dodoma, tukio ambalo limefanyika chuo Kikuu cha Dodoma.

“Tuwaamini wenzetu pale wanapotuambia wananyanyaswa, tuwasikilize na tuwasaidie, na hata tukiwa nyumbani tuwe wasikivu kwa watoto, wakituambia wanafanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia tufuatilie kwa ukaribu na kuchukua hatua za kisheria, tuache kumaliza masuala ya ukatili kifamilia kwani watendaji wataendelea kufanya vitendo hivyo.” Alisema.

Dkt. Chana ameongeza kuwa “ukatili wa kijinsia ni moja ya changamoto kubwa inayorudisha nyuma juhudi za kutambua usawa wa binadamu na utu wa mwanamke katika dunia ya leo, ni zao la mtizamo usio sahihi uliojengeka kwenye mila na desturi katika jamii unaomchukulia mwanamke kama mali ya mwanaume na kwamba ni kiumbe aliyeumbwa kutekeleza utashi wa mwanaume.”

Wakati Tanzania ikifanya Maadhimisho ya kimataifa ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia takwimu zinaonesha kuwepo kwa ongezeko la matukio ya ukatili huo hapa nchini. Ongezeko hilo linatokana na sababu mbalimbali ikiwemo jamii kuwa na uelewa zaidi juu ya madhara yatokanayo na ukatili wa kijinsia na kutoa taarifa za matukio ya ukatili huo katika Madawati ya Jinsia.

Sababu zingine ni mmomonyoko wa maadili, hali ngumu ya maisha ambayo huleta msongo wa mawazo kwa baadhi ya watu na kujikuta wakitenda matukio hayo. Sababu nyingine ni mila na tamaduni kandamizi, kushamiri kwa mfumo dume katika jamii zetu, matumizi mabaya ya teknolojia ambayo kwa kiasi kikubwa yamekuwa yakisababisha vijana kufanya vitendo vya kikatili hasa ubakaji wa watoto na wanawake lakini pia kulawiti.

Katika kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia nchini Dkt. Chana amesema Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji haki kwa wananchi hususan wanawake, watoto na makundi maalum ikiwa ni pamoja na kutunga sheria mbalimbali, kufanya maboresho ya mara kwa mara ya sheria, kanuni, miongozo na hata sera zinazosimamia usawa na ulinzi wa makundi mbalimbali.

Aidha, Serikali inayo mikakati mbalimbali ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia akiitaja moja ya mikakati hiyo kuwa ni Kampeni Kabambe ya Huduma za Msaada wa Kisheria iitwayo Mama Samia Legal Aid Camapign ambayo inatekelezwa na Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Wadau wa masuala ya upatikanaji haki hapa nchini.

Amevipongeza vyombo vya utoaji haki kuhakikisha washukiwa wote wa vitendo vya ukatili wa kijinsia wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria, kushughulikia mashauri kwa wakati na hivyo kesi kuhitimishwa ndani ya muda mfupi.

Dkt. Chana amelishukuru Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), kwa kushirikiana na Wizara na Chuo Kikuu cha Dodoma katika kuandaa maadhimisho hayo. Amemtaka Makamu Mkuu wa Chuo cha Dodoma Prof. Lughano Kusiluka na Amidi wa Shule ya Sheria Dkt. Ines Kajiru kuendelea kuwajenga wanafunzi wao katika misingi ya kuwa mabalozi wema wa masuala ya ukatili wa kijinsia.

Aidha, ameaomba Wadau wa Maendeleo na Mashirika yanayotetea haki za wanawake na watoto kuongeza mashirikiano ya muda mrefu na usaidizi katika kuunga juhudi za Serikali katika kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia miongoni mwa jamii huku akiyataka mashirika hayo kujikita zaidi katika maeneo ya pembezoni kwani kule ndipo kwenye changamoto zaidi kutokana na ukweli kwamba, elimu ya masuala haya bado haijafika vya kutosha kwahiyo jamii bado inaamini katika mila na desturi.



Meza Kuu kwenye picha ya pamoja na baadhi ya Wawakilishi wa Wizara na Taasisi kwenye hafla ya kufungua Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, tarehe 06 Desemba, 2023 Jijini Dodoma.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana alipotembelea Dawati la Jinsia Chuo Kikuu cha Dodoma kabla ya kufungua siku 16 za kupinga ukatili ya kijinsia, tarehe 06 Desemba, 2023

# DKT. CHANA ATAKA WATUMISHI KUFANYA KAZI KWA KUZINGATIA MASLAHI YA TAIFA



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akihutubia wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya RITA, 22 Desemba, 2023 Jijini Arusha.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akihutubia wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya RITA, 22 Desemba, 2023 Jijini Arusha.

**Na William Mabusi**
– WKS Dodoma.

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana ametoa wito kwa watumishi wa umma kufanya kazi kwa weledi na uadilifu kwa kuzingata maslahi mapana ya Serikali na Taifa kwa ujumla.

Dkt. Chana ameyasema hayo wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa ofisi ya RITA tarehe 22 Desemba, 2023 linalofanyika Jijini Arusha. Baraza hilo linafanyika ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya ajira na Mahusiano kazini.

Amesema, "huduma ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu na Takwimu mnazotoa ni huduma zinazowagusa wananchi moja kwa moja. Hivyo, mkiwa wafanyakazi mlioaminiwa na Serikali ya Tanzania endeleeni kutekeleza majukumu yenu kwa weledi na uadilifu kwa kuzingata maslahi mapana ya Serikali na Taifa kwa ujumla."

Amezitaja huduma zinazotolewa na RITA kuwa ni pamoja na usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Watoto wa kuasili, Usimamizi wa mirathi, Usajili wa Bodi za Wadhamini, Kuandika na kuhifadhi wosia miongoni mwa zingine.

Dkt. Chana amemshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utekelezaji wa falsafa ya R 4 hususan kwenye maboresho ya huduma zinazotolewa na Wakala wa RITA huku akiuagiza uongozi wa RITA kushughulikia changamoto mbalimbali za watumishi. "shughulikieni changamoto za wafanyakazi waweze kufanya kazi kwa furaha na ufanisi kwa kuwa mtumishi akiwa na furaha katika kazi ni wazi utendaji wake utakuwa wenye tija."

Aidha, Dkt. Chana amehimiza umoja miongoni mwa wafanyakazi wa ofisi ya RITA akiwataka wajenge Utumishi wa Umma wenye kuzingatia Kanuni za Maadili ya Utumishi, kupinga rushwa na kuheshimu sheria.

# MAADHIMISHO YA SIKU YA MAADILI NA HAKI ZA BINADAMU YAZINDULIWA.



**Na George Mwakyembe**
– WKS Dodoma.

Maadhimisho ya siku ya Maadili na haki za binadamu yalizinduliwa rasmi tarehe 03 Desemba, 2023 katika hafla iliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma. Kauli mbiu ya maadhimisho hayo ni "Zingatia Maadili, Utu, Uhuru, na Haki kwa watu wote kwa maendeleo endelevu"

Akizindua maadhimisho hayo Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana alisema kuwa maadhimisho hayo yana lengo la kuwakumbusha viongozi, watumishi na wananchi kwa ujumla wake juu ya dhana nzima ya kuwa na maadili, kukwepa vitendo vya rushwa, kuzingatia haki za binadamu, kufuata taratibu na kanuni mbalimbali za nchi jambo ambalo litaileta maendeleo katika jamii na Serikali kwa ujumla.

Mhe. Pindi aliendelea kusema kuwa jukumu la Serikali ni kuhakikisha kuwa inawaletea wananchi maendeleo hivyo usimamizi wa Maadili na mapambano dhidi ya rushwa na masuala ambayo lazima yatiliwe mkazo ili kuwa na viongozi, watumishi na jamii yenye madili na itakayokua mstari wa mbele katika kukwepa vitendo vya rushwa jambo ambalo litasaidia usimamizi na matumizi mazuri ya rasilimali za nchi.

"Serikali yetu chini ya Rais wetu mpendwa Mhe. Samia Suluhu Hassan imekua ikipeleka fedha nyingi katika miradi mbalimbali lakini fedha hizo zimekua zikiishia katika mifuko ya watu wachache waliokosa maadili na kukwamisha juhudi za Serikali yetu, niwaase ndugu zangu tushiriki kwa pamoja kusimamia maadili na kupinga vitendo vya rushwa na tuiunge Serikali yetu mkono ili sote tufurahie rasilimali za nchi yetu" alisema.

Pamoja na hayo Mhe. Pindi alisema kuwa maadhimiso ya siku ya maadili na haki za binadamu yanapaswa kuwa endelevu "Kuadhimisha siku hii kunatupa fursa ya kujitathmini ni wapi tulipotoka ni wapi tulipo na ni wapi tunaelekea katika suala zima la Maadili" alisema.

Katika hatua nyingine Mhe. Pindi alitumia fursa hiyo kuwaasa baadhi ya watendaji wa serikali wasiofuata taratibu katika kutoa haki badala yake wanadai rushwa kwa njia mbalimbali jambo ambalo ni utomvu wa maadili "wapo baadhi ya watendaji wenzangu wanaotumia vyeo na madaraka yao vibaya kwa kudai rushwa kwa njia mbalimbali na kukiuka haki za binadamu kwa kutokutoa maamuzi ya haki, tunapaswa kujitafakari na kuzingatia viapo vyetu" alisema.

Shuhuli mbalimbali zitafanyika katika kuadhimisha Siku ya Maadili na Haki za Binadamu kwa mwaka 2023 ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa umaa kupitia vyombo mbalimbali vya habari nchini, jukwaa la wadau wa masuala ya rushwa, wiki ya kutoa huduma kwa jamii pamoja na kilele cha maadhimisho hayo tarehe 10 Desemba,2023.

Maadhimisho ya siku ya Maadili na haki za binadamu nchini, imetokana na siku mbili tofauti ambazo huadhimishwa kimataifa ambazo ni Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Rushwa pamoja na Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu ambapo kuanzia mwaka 2016 Serikali iliamua kuadhimisha siku hizi kwa pamoja hivyo mwaka huu ni wa saba (7) kwa maadhimisho haya kufanyika kwa pamoja.

Maadhimisho hayo huratibiwa na taasisi zinazosimamia utawala bora ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Wizara ya Katiba na Sheria, Taasisi ya Kuzuia na kupambana na Rushwa, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Tume ya Utumishi wa Umma, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali pamoja na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.Maadhimisho hayo yamehudhuriwa na wananchi kutoka mikoa mbalimbali nchini yakiambatana na mbio ndefu na fupi zilizoitwa Sepesha Rushwa Marathoni zikiwa na lengo la kupinga vitendo vya rushwa nchini. Kauli mbiu ya maadhimisho hayo ni ***"Zingatia Maadili, Utu, Uhuru na Haki kwa watu wote kwa Maendeleo ya Endelevu."***

Maadhimisho hayo yanaadhimishwa sambamba na maadhimisho ya miaka 75 ya Tamko la Haki za Binadamu ***(Universal Declaration of Human Rights)*** ambayo huadhimishwa kila tarehe 10 Desemba ya kila mwaka hivyo siku hiyo ndiyo itakuwa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Kitaifa.






Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa akitoa hotuba kwenye Kilele cha Maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu yaliyofanyika leo tarehe 10 Desemba 2023 Jijini Dodoma

# WANANCHI WATAKIWA KUUNGA MKONO JITIHADA ZA SERIKALI KUPINGA UKIUKWAJI WA HAKI ZA BINADAMU

**Na George Mwakyembe & William Mabusi**
– WKS Dodoma.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) ametoa wito kwa wananchi kuunga mkono jitihada za Serikali ili kuleta matokeo chanya katika kupinga vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu, rushwa na mmomonyoko wa maadili akiwataka wanachi wanapobaini vitendo hivyo kutoa tarifa kwenye vyombo vya sheria ili wahusika wachukuliwe hatua.

Waziri Mkuu ameyasema hayo alipokuwa akihutubia wakati wa kufunga maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Kitaifa leo tarehe 10 Desemba, 2023 hafla iliyofanyika Viwanja vya Nyerere Square Jijini Dodoma yakiongozwa na kauli mbiu isemayo “Zingatia maadili, utu, uhuru na haki kwa watu wote kwa maendeleo endelevu.”

Mhe. Majaliwa amesema “Wananchi ninyi ni wadau wakubwa wa kutokomeza rushwa, kukomesha vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu. Ili nchi yetu isiwe na vitendo vya rushwa, isiwe na vitendi vya ukiukwaji wa haki za binadamu nyie mnapaswa kufichua matendo hayo na kupeleka taarifa kwenye vyombo husika katika kusimamia na kudhibiti matendo hayo, mwananchi usikubali kutoa rushwa popote unapotakiwa kupata huduma.”
Katika kukabiliana na dhuruma ya rushwa amesema nchi imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwa na Mkakati wa Kitaifa wa kupambana na rushwa ambao hadi sasa umetekelezwa kwa Awamu Tatu na katika hafla hiyo alizindua Mkakati wa Nne wa kupambana na rushwa ili uanze kutumika rasmi huku akiagiza elimu ya utekelezaji wa Mkakati huo iendelee kutolewa ili kuwawezesha wadau wote kuwa na uelewa wa pamoja katika kushiriki kutekeleza Mkakati huo.

Awali akitoa salaam kwenye hafla hiyo Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) amezishukuru
Wizara na Taaasisi ambazo kwa wiki nzima zimeshiriki kutoa elimu juu ya haki za binadamu, rushwa, vitendo vya ukatili wa kijinsia. Aidha, Wizara hizo pia zilitoa huduma na kutatua malalamiko kutoka kwa wananchi. Amevishukuru Vyombo vya Habari kwa kurusha vipindi kwenye redio na TV na kutoa taarifa za maadhimisho hayo tangu yalipozinduliwa tarehe 3 Desemba, 2023.

Maadhimisho hayo yanaenda sambamba na maadhimisho ya miaka 75 ya Tamko la Dunia kuhusu haki za binadamu la mwaka 1948 ambapo Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa iliyoridhia mikataba mbalimbali ikiwemo ya haki za binadamu ya Kikanda na Kimataifa.




Mgeni Rasmi Mhe. Kassim Majaliwa akiwa na viongozi wengine Meza Kuu kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu yaliyofanyika tarehe 10 Desemba, 2023 Jijini Dodoma.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Pindi Chana akitoa neno la utambulisho kwenye kilele cha Maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu yaliyofanyika tarehe 10 Desemba, 2023 Jijini Dodoma

# Ujenzi wa Jengo la Wizara Wafikia Asilimia 80



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Dkt. Khatibu Kazungu akishauri jambo alipotembelea na kukagua ujenzi wa jengo la Wizara, tarehe 29 Desemba, 2023 Mji wa Serikali Mtumba.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Dkt. Khatibu Kazungu akitembelea na kukagua ujenzi wa jengo la Wizara, tarehe 29 Desemba, 2023 Mji wa Serikali Mtumba



Mkandarasi Nasiri Nassoro akifafanua jambo wakati akitoa maelezo ya maendeleo ya ujenzi wa jengo la Wizara kwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Dkt. Khatibu Kazungu alipotembelea na kukagua ujenzi huo, tarehe 29 Desemba, 2023 Mji wa Serikali Mtumba.

**William Mabusi**
– WKS Dodoma.

Ujenzi wa jengo la Wizara ya Katiba na Sheria linalojengwa Mji wa Serikali Mtumba limefikia asilimia themanini (80).

Taarifa hiyo imetolewa na Bw. Ibrahimu Chatila Mtaalam Mwelekezi kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Dkt. Khatibu Kazungu tarehe 29 Desemba, 2023 alipotembelea maendeleo ya ujenzi huo. Aidha, Bw. Chatila amemtaka Mkandarasi wa ujenzi huo SUMA JKT kutobweteka kwa hiyo asilimia themanini kwani mradi huo ni miongoni mwa miradi ambayo Mkandarasi analipwa kwa wakati.

Akitoa maelekezo baada kukagua maendeleo ya ujenzi huo Dkt. Kazungu amesema "jitihada mlizoonesha hadi kufikia hatua hii ongezeni bidii na hasa baada ya kupokea vifaa vyenu vya ujenzi ambavyo bado viko bandarini."

Kabla ya kufanya ukaguzi wa ujenzi Dkt. Kazungu akiwa na Menejimenti ya Wizara hiyo walikutana na kufanya mazungumzo na Wakandarasi kutoka SUMA JKT na Wataalam wa Majengo kutoka TBA.

# Matukio Katika Picha



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akipiga picha aliposhiriki kufungua Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, tarehe 06 Desemba, 2023 Jijini Dodoma.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akishiriki katika zoezi la kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa Watoto wa Umri chini ya miaka mitano, Desemba 08, 2023 katika viwanja vya Mbagala Zakhiem Jijini Dar es Salaam.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiwa katika banda la Wizara ya Katiba na Sheria kwenye Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu yaliyofanyika tarehe 10 Desemba, 2023 Jijini Dodoma.







Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akisalimiana na viongozi mbalimbali wa vyama kabla ya Kuanza kwa mkutano maalumu wa wa Baraza la Vyama vya Siasa Unaoshirikisha Wadau wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa Kujadili Miswada ya Sheria za Uchaguzi na Sheria za Vyama vya Siasa 03/01/2024.



Washiriki siku ya kufungua Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, wakimkaribisha ukumbini Mgeni Rasmi Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana tarehe 06 Desemba, 2023 Jijini Dodoma.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akipata maelezo kutoka kwa Amidi wa Shule ya Sheria Dkt. Ines Kajiru kuhusu Kliniki ya Sheria Chuo Kikuu cha Dodoma, tarehe 06 Desemba, 2023



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana kwenye picha ya pamoja na baadhi ya viongozi walioshiriki hafla ya kufungua Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, tarehe 06 Desemba, 2023 Jijini Dodoma.




Rais wa serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Hussein Ali Mwinyi akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe alipozindua Kikao cha kawaida cha 77 cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Jijini Arusha tarehe 20/10/2023.




Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana (kulia) akisalimiana na Mhe. Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora wakati walipokutana Arusha kwenye Kikao cha kawaida cha 77 cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

